TANGAZO LA SERIKALI Na. 497 la Tarehe 21/7/2023

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 222)*

KANUNI ZA VIFAA VYA UOKOZI NA MIPANGILIO ZA MWAKA 2023

## MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.
4. Rejea ya mkataba.

SEHEMU YA PILI
AINA ZA MELI NA IDHINI YA MIPANGILIO NA VIFAA VYA UOKOZI

5. Madaraja ya meli.
6. Idhini na kubadilishwa.
7. Misamaha.

SEHEMU YA TATU
MASHARTI YA MELI ZILIZOJENGWA KABLA YA TAREHE 1 JULAI, 1988 NA ZINAZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA

8. Matumizi.
9. Masharti kwa meli zilizojengwa kabla ya Tarehe 1 Julai 1988.
10. Ubadilishwaji wa vifaa vya uokozi wa maisha na mpangilio.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI YA MELI ZILIZOJENGWA KABLA YA TAREHE 1 JULAI, 1988 NA ZISIZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA

11. Matumizi.
12. Masharti kwa meli zilizojengwa kabla ya Tarehe 1 Julai 1988.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI KWA MELI MPYA ZINAZOSHIRIKI SAFARI ZA KIMATAIFA

13. Matumizi.
14. Masharti kwa meli mpya zinazoshiriki safari za kimataifa.
15. Ubunifu mbadala na mipangilio kwa meli mpya.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI KWA MELI MPYA ZISIZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA NA MELI MPYA ZINAZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA AMBAZO SEHEMU B YA SURA YA III YA MKATABA WA USALAMA HAITUMIKI

16. Matumizi.
17. Masharti kwa meli mpya.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

18. Uzuiaji.
19. Tathmini na utoaji wa taarifa.
20. Makosa na adhabu.
21. Kushughulikia malalamiko.

---

JEDWALI

---

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

---

# KANUNI

---

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 222)*

## KANUNI ZA VIFAA VYA UOKOZI NA MIPANGILIO ZA MWAKA 2023

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Vifaa vya Uokozi na Mpangilio za Mwaka 2023.

Matumizi

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika-
(a) kwa ajili ya kutekeleza Sura ya III ya Mkataba wa Usalama;
(b) kwa meli za Tanzania, popote zilipo;
(c) kwa meli sizizo za Tanzania wakati zinapokuwa katika maji ya Tanzania; na
(d) kwa meli ya starehe ya Tanzania inayofanya kazi kwa kukodi au malipo au kwa aina nyingine yoyote ya malipo ya kifedha.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Kanuni hizi hazitatumika kwa-
(a) meli za kivita au msaada wa kijeshi;
(b) meli zinazomilikiwa au kutumiwa na Serikali na kujihusisha na shughuli za kiserikali zisizo za kibiashara;
(c) meli za abiria Daraja la III, IV, V, VI na VI(A);
(d) meli za mbao zilizojengwa kiasili;
(e) meli za uvuvi;
(f) meli zisizo za Tanzania ambazo ni meli za starehe;
(g) meli zenye urefu usiopungua mita 24 au tani 50 za jumla; na

(h) meli isiyo ya Tanzania ambayo inapeperusha bendera ya Nchi ambayo si mwanachama wa Mkataba wa Usalama na isingekuwa katika maji ya Tanzania isipokuwa kwa dhoruba ya hali ya hewa au mazingira yoyote ambayo nahodha, mmiliki au mkodishaji asingeweza kuzuia.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"abiria" maana yake ni mtu yeyote aliyebebwa kwenye meli tofauti na-

(a) mtu aliyeariliwa au anaejihusisha katika nafasi yoyote katika shughuli za melini;

(b) mtu aliye ndani ya meli kwa sababu ya ruhusa iliyotolewa na nahodha kufanya shughuli za kuibua meli, dhoruba au watu wengine au kwa sababu nyingine yoyote ambazo nahodha, mmiliki, au mkodishaji, kama yupo, asingeweza kuzuia au kuepusha;

(c) mtoto chini ya mwaka mmoja;

"abiria maalum wa biashara" maana yake ni abiria anayesafirishwa kwa biashara maalum katika sakafu wazi ya meli, sakafu ya juu, au kati ya sakafu zinazoweza kubeba zaidi ya abiria nane; na

"bahari" maana yake ni mlango wa mto au mkono wa bahari tofauti na aina A, B, C au D ya maji;

"chombo cha starehe" maana yake ni-

(a) chombo chochote ikijumuisha boti za kuzamia ambacho wakati wa matumizi yake-

(i) kinamilikiwa na mtu au watu binafsi na kinatumika kwa ajili ya michezo pekee au starehe ya mmiliki au wanafamilia au marafiki wa mmiliki; au

(ii) kinamilikiwa na kampuni ambapo watu wanaokitumia ni waajiriwa, maafisa, au wadau wa kampuni, au wana familia au marafiki;

(b) chombo kilichopo safarini ambacho mmiliki wake hapokei pesa kutokana na uendeshaji wa

chombo hicho au kubeba mtu yeyote, tofauti na michango ya moja kwa moja ya gharama za uendeshaji wa chombo zilizotumika wakati wa safari, au chombo chochote kinachomilikiwa moja kwa moja au kwa niaba ya klabu iliyoanzishwa kwa malengo ya michezo au starehe ambacho wakati wa matumizi yake kinatumiwa kwa madhumuni pekee ya michezo au starehe kwa wanachama wa klabu au wana familia wao wa karibu, na kwa matumizi ambayo tozo zake hulipwa katika mfuko wa klabu na kutumika kwa matumizi ya jumla ya klabu;

"hatua sawa ya ujenzi" maana yake ni hatua ambayo-

(a) ujenzi unaotambulika kwa meli maalum unaanza; na

(b) uundwaji wa meli umeanza kwa kujumuisha angalau tani 50 au 1% ya uzito unaotarajiwa wa vifaa vya ujenzi, chochote kitakachokuwa kidogo;

TS. Na. 63 la 2019

"Kundi A, B, C au D" maana yake ni maji yaliyoanishwa katika Kanuni za Ukomo wa Upakiaji za Usafiri Majini;

"maili" maana yake ni notiko maili za kimataifa za mita 1,852;

"meli maalum ya abiria ya biashara" maana yake ni meli ya abiria inayoendeshwa kimitambo ambayo hubeba idadi kubwa ya abiria maalum wa biashara;

"meli mpya" maana yake ni meli ambayo nguzo yake imesimamishwa, au iko katika hatua sawa ya ujenzi, tangu tarehe 1 Julai 1998;

"meli ya abiria" maana yake ni meli iliyojengwa kwa, au ambayo kimsingi au katika matukio maalum kubeba zaidi ya abiria 12 na inajumuisha meli ambayo imetolewa kwa usafiri au burudani kwa wageni katika taasisi yoyote, hoteli, nyumba za kupumzikia wageni, nyumba za wageni au matumizi mengine;

"Mkataba wa Usalama" maana yake ni Mkataba wa

Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa mwaka 1974 na Itifaki zake za mwaka 1978 na 1988, pamoja na marekebisho yake, au mbadala wake kama utakavyotumika Tanzania;

Sura ya 415

"Msajili" maana yake ni Msajili aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 31 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"Nchi ya Mkataba wa Usalama" maana yake ni Nchi ambayo Serikali yake imeridhia matumizi ya Mkataba wa Usalama na ambayo haijajitoa katika Mkataba huo, au eneo la Nchi ambalo Mkataba huo unatumika na kuendelea kutumika;

"Notisi ya Usafiri Majini" maana yake ni Notisi ya Usafiri Majini inayotolewa na Msajili na inajumuisha rejea ya nyaraka yoyote inayorekebisha au kubadili Notisi hiyo;

"safari fupi ya kimataifa" maana yake ni safari ya kimataifa-

(a) ambayo meli haiko zaidi ya maili 200 za nautiki kutoka bandari au mahali ambapo abiria na wafanyakazi wanaweza kuwekwa salama; na

(b) ambayo haizidi maili 600 za nautiki kati ya bandari ya kuondokea na mwisho wa safari, bila kuzingatia mabadiliko yoyote ya njia katika safari yake kutokana na hali mbaya ya hewa au mazingira yoyote ambayo nahodha, mmiliki au mkodishaji wa meli asingeweza kuzuia au kuepusha;

"safari ya kimataifa" maana yake ni safari kati ya-

(a) bandari ya Tanzania na bandari iliyo nje ya Tanzania; au

(b) bandari katika Nchi ya Mkataba, isipokuwa Tanzania, na bandari katika Nchi yoyote au mipaka, iwe au isiwe Nchi ya Mkataba, iliyo nje ya Tanzania;

Sura ya 165

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Usafiri Majini;

Sura ya 415

"Shirika" maana yake ni Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania lililoanzishwa chini ya kifungu cha 4 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania;

"Sura ya III" maana yake ni Sura ya III ya Mkataba wa Kimataifa wa Usalama wa Maisha Baharini wa 1974; na

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana ya masuala ya usafiri majini.

Rejea ya mkataba

4.-(1) Katika Kanuni hizi, rejea yoyote ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama itatafsiriwa-

(a) kama rejea ya Sura ya III ilivyorekebishwa; na

(b) pale ambapo Sura ya III imebadilishwa, rejea ya mabadiliko.

(2) Kwa madhumi ya kifungu kidogo cha (1), Sura ya III itakuwa imerekebishwa au kubadilishwa kama marekebisho au mabadiliko yamefanyika sawa na Ibara ya VIII ya Mkataba.

(3) Marekebisho au mabadiliko ya Sura ya III yataanza kutumika wakati marekebisho au mabadiliko hayo yamezingatia matakwa ya Ibara ya VIII ya Mkataba.

## SEHEMU YA PILI
## MADARAJA YA MELI NA IDHINI YA VIFAA VYA UOKOZI NA MPANGILIO

Madara ya meli

5. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, madaraja ya meli yatakua kama yalivyoanishwa katika Jedwali la Kanuni hizi.

Idhini na kubadilishwa

6.-(1) Vifaa vya uokozi vilivyowekwa katika meli ya Tanzania vitaidhinishwa na Msajili au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Msajili.

(2) Msajili au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Msajili anaweza kutoa idhini kuhusiana na meli ya Tanzania kwa suala lolote katika Sura ya III ya Mkataba wa Usalama endapo inahitaji:

(a) kuidhinishwa na Nchi ya usajili wa meli ambayo meli inastahili kupeperusha bendera

yake;

(b) kukidhi matakwa ya Nchi ya usajili wa meli; na

(c) kukubalika na Nchi ya Usajili wa meli.

(3) Idhini iliyotolewa chini ya kanuni ndogo ya (1) au (2) inaweza, kwa kutoa notisi kuruhusiwa kuendelezwa, kubadilishwa au kufutwa.

(4) Idhini, mwendelezo, mabadiliko au kufutwa kulikotolewa chini ya kanuni hii:

(a) kutakuwa kwa maandishi;

(b) kutabainisha tarehe ya kuanza kutumika; na

(c) kutabainisha masharti, kama yapo, ya kutolewa kwake.

(5) Sharti kwamba idhini, mwendelezo, mabadiliko au kufutwa chini ya kanuni hii kuwa kwa maandishi litatimia pale ambapo maandishi ya idhini:

(a) yamewekwa kielektroniki;

(b) yamepokelewa katika mfumo unaosomeka; na

(c) yanafaa kutumika kwa marejeo yanayofuata.

(6) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (7), kifaa chochote cha uokozi wa maisha chenye tarehe ya ukomo wa matumizi-

(a) kitakoma kuidhinishwa kwa madhumuni ya Kanuni hizi katika ukomo wa tarehe ya matumizi; na

(b) kitabadilishwa wakati au kabla ya tarehe ya ukomo.

(7) Kifungashio cha dharura cha chombo cha uokozi, kilichokaguliwa wakati ukarabati wa mwaka wa chombo cha uokozi na kina maisha ya miezi sita iliyosalia kabla ya tarehe ya ukomo wakati wa muda wa ukaguzi kinaweza kuachwa mpaka kipindi cha ukarabati wa mwaka unaofuata.

(8) Msajili atajiridhisha kuwa vifaa vya ukozi wa maisha na mpangilio unazingatia masharti ya Kanuni hizi na za Kimataifa za vifaa vya uokozi wa maisha, kabla ya kukubali vifaa na mpangilio ya uokoaji wa maisha ambavyo havikuwa vimeidhinishwa na msajili hapo awali.

Misamaha

7.-(1) Msajili anaweza kusamehe-

(a) meli au aina za meli ambazo, wakati wa safari, haziendi umbali zaidi ya maili 20 kutoka nchi kavu ya karibu, na pale ambapo msajili ameridhika kwamba eneo la kujistihili na hali ya safari hiyo inalazimisha kutokuwa na umuhimu au ulazima wa kutumia masharti ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama;

(b) meli ambayo kwa kawaida haifanyi safari za kimataifa lakini katika uhitaji wa kipekee, inatakiwa kufanya safari moja ya kimataifa;

(c) meli yenye muundo wa vifaa vya aina ya riwaya kama tafiti kutoka vifaa hivyo na mjumuisho wake katika meli inayofanya safari za Kimataifa unaweza kuzuiliwa pale ambapo meli itapaswa kukidhi matakwa ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama.

(2) Msajili anaweza, katika mazingira ya kipekee ambayo hayajaainishwa katika kanuni ndogo ya (1), kusamehe kutumika kwa masharti yoyote ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama, kwa meli au aina za meli endapo atajiridhisha kwamba uzingatiaji wa masharti hayo hautekelezeki au hauna mantiki kuhusiana na meli au aina za meli hizo.

(3) Msamaha chini ya kanuni hii, unaweza kutolewa kwa kuzingatia masharti ya usalama, kama itakavyoonekana inafaa na Msajili kwa lengo la kuhakikisha usalama wa jumla wa meli.

(4) Msamaha uliotolewa chini ya kanuni hii unaweza, kwa kutolewa notisi ya msingi, kurekebishwa au kufutwa.

(5) Msamaha, mabadiliko au kufutwa kulikotolewa chini ya kanuni hii kutapaswa-

(a) kuwa katika maandishi;

(b) kufafanua tarehe ambayo utaanza kutumika; na

(c) kuainisha masharti yaliyotolewa, kama yapo.

(6) Sharti kwamba msahama, mabadiliko au

kufutwa kulikotolewa chini ya kanuni hii kuwa kwa maandishi litatimia pale ambapo maandishi ya idhini-

(a) yamewekwa kwa njia ya kielektroniki;

(b) yamepokelewa katika mfumo unaosomeka; na

(c) yanafaa kutumika kwa marejeo yanayofuata.

(7) Pale ambapo msahama umetolewa kwa kuzingatia masharti ya usalama, msamaha utakoma kutumika endapo masharti hayo hayatazingatiwa.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI KWA MELI ZILIZOJENGWA KABLA YA TAREHE 1 JULAI 1998 ZINAZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA

Matumizi

8. Sehemu hii inatumika kwa meli za Daraja la I, II, VII, VII(A), VII(T), VIII, VIII(T), IX, XI na XII, ambazo nguzo zilikuwa zimewekwa au zilikuwa katika hatua sawa ya ujenzi, kabla ya 1 Julai, 1998 kufanya safari za kimataifa.

Masharti kwa meli zilizojengwa kabla ya tarehe 1 Julai, 1998

9.-(1) Meli ambayo sehemu hii inatumika itazingatia kila sharti la Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama inayotumika kwake, isipokuwa kwa meli za Daraja la XI na XII.

(2) Meli zilizojengwa kabla ya tarehe 1 Julai, 1998 zitakuwa chini ya masharti maalum ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama, ikijumuisha kanuni zinazotumika kwa "meli zote".

(3) Maneno "meli zote" maana yake ni meli zilizojengwa kabla, mnamo au baada ya tarehe 1 Julai, 1998; maneno meli zote za abiria na meli zote za mizigo yatatafsiriwa ipasavyo.

Ubadilishaji wa vifaa vya uokozi wa maisha na mpangilio

10.-(1) Kanuni hii haitumiki kwa meli za Daraja la XI na XII.

(2) Pale ambapo katika meli Sehemu hii inatumika-

(a) vifaa vya uokozi wa maisha au mpangilio unabadilishwa; au

(b) meli inafanyiwa ukarabati, mabadiliko au uboreshaji mkubwa wa muundo unaohusisha

ubadilishaji wa, nyongeza yoyote kwa, vifaa vyake vya uokozi wa maisha au mpangilio,

kubadilishwa au kuongezwa kwa vifaa vya uokoaji wa maisha au mpangilio kwa namna ilivyozoeleka, kutapaswa kuzingatia masharti ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama.

(3) Pale ambapo-

(a) chombo cha uokoaji, tofauti na kifaa cha uokozi wa maisha kinachoelea kimebadilishwa lakini kifaa chake cha kutumbukiza majini hakijabadilishwa; au

(b) kifaa cha kutumbukiza chombo cha uokoaji majini tofauti na chombo cha uokoaji, kimebadilishwa lakini chombo cha uokoaji hakijabadilishwa,

chombo cha uokoaji au chombo cha kutumbukiza majini, kama itakavyokuwa, kitapaswa kuwa cha aina ile iliyobadilishwa.

## SEHEMU YA NNE
## MASHARTI KWA MELI ZILIZOJENGWA KABLA YA TAREHE 1 JULAI 1998 ZISIZOFANYA SAFARI ZA KITAIFA

Matumizi

11. Sehemu hii inatumika kwa meli za Daraja la II(A), VII(A), VIII(A), VIII(A)(T), IX, IX(A), IX(A)(T), XI na XII, ambazo nguzo zilikuwa zimewekwa au zilikuwa katika hatua sawa ya ujenzi, kabla ya tarehe 1 Julai, 1998 zisizofanya safari za kimataifa.

Masharti kwa meli zilizojengwa kabla ya tarehe 1 Julai, 1998

12. Meli ambayo sehemu hii inatumika itazingatia kila sharti la Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama inayotumika kwake.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI KWA MELI MPYA ZINAZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA

Matumizi

13. Sehemu hii inatumika kwa meli mpya za Daraja la I, II, VII, VII(T), VIII, VIII(T), IX, XI na XII

zinazofanya safari za kimataifa.

Masharti kwa meli mpya zinazofanya safari za kimataifa

14. Meli mpya za Daraja la I, II, VII, VII(T), VIII, VIII(T) au IX, wakati zinapofanya safari za kimataifa, zitazingatia mashatri yote ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama yanayotumika kwake.

Ubunifu mbadala na mipangilio kwa meli mpya

15.-(1) Vifaa vya uokozi wa maisha na mipangilio kwa meli mpya ambazo kanuni ya 14 inatumika, vinaweza kutofuata masharti ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama, ikizingatiwa kwamba ubunifu mbadala na mipangilio inakidhi masharti ya Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama na kutoa kiwango sawa cha usalama.

(2) Kuhusiana na meli ambazo kanuni ya 14 inatumika-

(a) ubunifu mbadala au mpangilio itafanyiwa uchambuzi wa uhandisi kwa mujibu wa aya ya 38.3 ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama kuhusiana na vipengele vya uchambuzi wa uhandisi; na

(b) nakala ya uchambuzi wa uhandisi itawasilisha kwa Shirika na mliki.

(3) Kuhusiana na ubunifu mbadala au mpangilio na uchambuzi wa uhandisi uliorejewa katika kifungu kidogo cha (2)-

(a) Shirika litatathmini na iwapo litajiridhisha kwamba masharti ya aya ya 38.3 cha Sura ya III ya Mkataba wa Usalama yamezingatiwa, litaidhinisha uchambuzi wa uhandisi; na

(b) marekebisho yoyote ya ubunifu mbadala au mpangilio yataidhinishwa na Shirika kwa kujiridhisha kuwa ubunifu mbadala au mpangilio ni angalau sawa na inavyohitajika na Kanuni hizi.

(4) Pale ambapo dhana na vikwazo vya uendeshaji vilivyotajwa katika ubunifu mbadala au mpangilio chini ya kanuni ndogo ya (2) vinabadilishwa, uchambuzi wa ziada wa uhandisi utafanyika kwa kuzingatia mabadiliko ya dhana na vikwazo vya

uendeshaji.

(5) Pale ambapo ubunifu mbadala au mpangilio uliotajwa chini ya kanuni ndogo ya (2) unahitaji marekebisho, utafanyiwa tathmini na kuidhinishwa na Shirika, endapo litajiridhisha kuwa ubunifu mbadala au mpangilio ni angalau sawa na inavyohitajika na Kanuni hizi.

(6) Idhini iliyotolewa chini ya kanuni hii inaweza, kwa kutolewa notisi ya msingi, kuendelea, kurekebishwa au kufutwa.

(7) Idhini ya kuendelea, kurekebishwa au kufutwa iliyotolewa chini ya kanuni hii-

(a) itakuwa kwa maandishi;

(b) itafafanua tarehe ambayo itaanza kutumika; na

(c) itafafanua masharti yaliyotolewa, kama yapo.

(8) Sharti kuwa idhini ya kuendelea, mabadiliko au kufutwa kulikorejewa chini ya kanuni hii, kuwa kwa maandishi litatimia pale ambapo maudhui ya idhini-

(a) yamewekwa kwa njia ya kielektroniki;

(b) yamepokelewa katika mfumo unaosomeka; na

(c) yanafaa kutumika kwa marejeo yanayofuata.

(9) Nakala ya idhini ya kuendelea au kubadilishwa iliyotolewa chini ya kanuni hii, na ambayo inathibitisha kuwa ubunifu mbadala au mpangilio umezingatia Sura ya III ya Mkataba wa Usalama, itabebwa ndani ya meli.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI KWA MELI MPYA ZINAZOFANYA SAFARI ZISIZO ZA KIMATAIFA NA MELI MPYA ZINAZOFANYA SAFARI ZA KIMATAIFA AMBAZO SEHEMU B YA SURA YA III YA MKATABA WA USALAMA HAITUMIKI

Matumizi

16.-(1) Sehemu hii inatumika kwa meli mpya za-

(a) daraja la II(A), VIII(A), VIII(A)(T), IX, IX(A), IX(A)(T), XI na XII ambazo hazifanyi safari za kimataifa; na

(b) daraja la I, II, VII, VII(T), VIII, VIII(T) na IX ambazo zinafanya safari za kimataifa lakini sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa

Usalama haitumiki.

(2) Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama haitatumiki kwa meli za mizigo chini ya tani za jumla 500 isipokuwa ikiwa imeelezwa vinginevyo katika Sura ya III.

(3) Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama itatumika kwa meli zote za abiria.

Masharti kwa meli mpya

17. Meli ambayo Sehemu hii inatumika inapaswa kuzingatia kila kifungu cha Sehemu B cha Sura ya III ya Mkataba wa Usalama inayotumika kwake.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

Uzuiaji

18.-(1) Meli ambayo haitazingatia masharti ya Kanuni hizi au Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama inaweza kuzuiliwa.

(2) Pale ambapo meli imezuiliwa chini ya kanuni ndogo ya (1), masharti ya kifungu cha 409 cha Sheria yatatumika, isipokuwa masharti yaliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (6) hayatatumika.

(3) Pale ambapo meli inapaswa kuzuiliwa chini ya kanuni hii, mtu anayeizuia meli hiyo atatoa notisi ya kuzuia kwa Nahodha ambayo-

(a) inaeleza sababu za kuwekwa kizuizini; na

(b) inahitaji masharti ya notisi kuzingatiwa hadi meli itakapoachiwa na mtu yeyote aliyetajwa chini ya kifungu cha 409 (1) cha Sheria.

(4) Pale ambapo meli nyingine ambayo siyo ya Tanzania imezuiliwa, Shirika litaifahamisha mara moja mamlaka ya nchi iliyosajili meli kwa maandishi.

(5) Pale ambapo haiwezekani kuijulisha mamlaka ya nchi iliyosajili meli kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (4), Shirika litaifahamisha ofisi ya Ubalozi wa mamlaka ya nchi iliyosajili meli, au endapo hakuna ofisi ya Ubalozi, mwakilishi wa karibu wa kidiplomasia wa nchi iliyosajili meli.

(6) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo za (4) na (5), "mamlaka ya nchi iliyosajili" kuhusiana na meli ina

maana nchi ambayo bendera yake inastahili kupeperushwa na meli husika.

Tathmini na utoaji wa taarifa

19.-(1) Msajili-

(a) atafanya tathmini ya masharti ya udhibiti yaliyomo katika Kanuni hizi;
(b) atandaa ripoti inayoainisha hitimisho la tathmini; na
(c) atawasilisha ripoti kwa Waziri.

(2) Ripoti ya kwanza chini ya kanuni hii itachapishwa kabla ya mwaka wa tano wa maadhimisho ya siku ambayo Kanuni hizi zitaanza kutumika.

(3) Ripoti zinazofuata zitachapishwa kwa kipindi kisichozidi miaka mitano.

(4) Ripoti iliyoandaliwa na kuwasilishwa chini ya kanuni hii-

(a) itaainisha malengo yanayokusudiwa kufikiwa na masharti ya udhibiti yaliyoanishwa chini ya kanuni ndogo ya (1)(a);
(b) itatathmini kiwango ambacho malengo hayo yanafikiwa;
(c) itatathmini endapo malengo yaliyoanishwa yana tija; na
(d) pale ambapo malengo yanatija, ripoti itatathmini kiwango ambacho yanaweza kufikiwa kwa njia nyingine inayohusisha masharti mepesi ya udhibiti.

Makosa na adhabu

20. Pale ambapo meli inaingia au kujaribu kuingia baharini au safari yoyote, au kuwasili ndani ya maji ya Tanzania, ikiwa imekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi au Sehemu B ya Sura ya III ya Mkataba wa Usalama unaotumika katika meli hiyo, mmiliki na nahodha kila mmoja atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua dola za Marekani elfu tano au kiwango kinacholingana katika shilingi za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili na kisichopungua mwaka mmoja au vyote kwa pamoja.

Ushughulikiaji wa malalamiko TS. Na. 338 la 2018

21. Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi uliotolewa chini ya Kanuni hizi anaweza kuwasilisha maombi ya mapitio kwa Shirika kwa mapitio kwa mujibu wa Kanuni za Ushughulikiaji wa Malalamiko za Wakala wa Meli Tanzania.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5)*

MADARAJA YA MELI

| *Meli za Abiria* | *Mchanganuo wa Madaraja ya Meli* |
|---|---|
| Daraja la I | meli zinazofanya safari zozote ndefu za kimataifa; |
| Daraja la II | meli zinazofanya safari fupi za kimataifa pekee; |
| Daraja la II(A) | meli zinazofanya safari za aina yoyote isipokuwa safari za kimataifa ambazo si-<br>(i) meli za Daraja la III hadi VI(A) kama zilivyotafsiriwa katika Kanuni za Ujenzi wa Meli za Abiria: Meli za Daraja la III hadi VI(A) za Mwaka 1998;<br>(ii) Meli za Daraja A, B, C au D kama zilivyotafsiriwa katika Kanuni za Meli za Abiria za Safari za Ndani za Mwaka 2000 na zinazofanya safari za ndani kwa madhumuni ya Kanuni hizo; |
| Daraja la III | meli zinazojihusisha na safari pekee nyakati zikiwa si zaidi ya maili 70 baharini kutoka eneo la kuondokea na si zaidi ya maili 18 kutoka pwani ya Jamhuri ya Muungano, na ambazo ziko bahari wakati wa hali nzuri ya hewa na kipindi kilichozuiliwa; |
| Daraja la IV | meli zinazofanya safari za maji katika Kundi A, B, C au D pekee; |
| Daraja la V | meli zinazofanya safari za maji katika Kundi A, B au C pekee; |

| | |
|---|---|
| Daraja la VI | meli zinazofanya safari pekee na abiria wasiozidi 250 ndani ya meli, baharini au katika maji ya Kundi A, B, C, au D, kwa namna yoyote katika hali nzuri ya hewa na kipindi cha muda kilichozuiliwa, katika wakati meli haipo umbali wa maili 15, isipokuwa katika maji ya kundi lolote la A, B, C, au D, kutoka katika eneo la kuondokea lisilo zaidi ya maili 3 kutoka nchi kavu. |
| Daraja la VI(A) | meli inayobeba abiria wasiozidi 50 kwa safari za umbali usiozidi maili 6 kwenda au kutoka katika jamii zilizotengwa kwenye visiwa au pwani ya Jamhuri ya Muungano na ambazo haziingii kwa umbali usiozidi maili 3 kutoka nchi kavu. |
| *Meli zisizo za abiria* | *Mchanganuo wa Madaraja ya Meli* |
| Daraja la VII | meli, isipokuwa meli za Daraja la I, VII(A), VII(T), XI, na XII, zinazofanya safari yoyote ndefu ambayo ni ya kimataifa; |
| Daraja la VII(A) | meli zinazohusika na kusindika samaki au kuzikausha samaki, na meli zinazotumika kubeba watu walioajiriwa katika viwanda vya kusindika au kukausha samaki; |
| Daraja la VII(T) | meli za mafuta zinazofanya safari zozote ndefu za kimataifa; |
| Daraja la VIII | meli, isipokua meli za daraja la II, VIII(T), IX, XI na XII, zinazofanya safari fupi za kimataifa pekee; |
| Daraja la VIII(A) | meli isipokuwa meli za Daraja la II(A) hadi VI(A) kwa pamoja, VIII(A)(T), IX, IX(A), IX(A)(T), XI na XII, zinazofanya safari pekee ambazo sio safari za kimataifa; |
| Daraja la VIII(T) | meli za mafuta zinafanya safari fupi za kimataifa pekee; |
| Daraja VIII(A)(T) | meli za mafuta zisizofanya safari fupi za kimataifa pekee; |
| Daraja la IX | tagi na meli ya tenda, isipokua meli za Daraja la II, II(A), III, VI na VI(A), ambazo zinaingia baharini lakini hazifanyi safari ndefu za kimataifa; |
| Daraja la IX(A) | meli, isipokuwa meli za Daraja la IV hadi VI kwa pamoja, ambazo haziingii baharini; |
| Daraja la IX(A)(T) | meli za mafuta ambazo haziingii baharini; |

| | |
|---|---|
| Daraja la XI | meli zinazoelea, tofauti na meli za uvuvi na meli za Daraja la XII, ambazo zinaingia baharini; |
| Daraja la XII | meli za starehe zevye urefu wa mita 13.7 au zaidi. |

Dodoma,
28 Juni, 2023

MAKAME M. MBARAWA,
*Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi*